



OFISI YA RAIS

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

MABADILIKO YA ENEO LA USAILI WA MAHOJIANO WA TAREHE

13 JUNI,2026 KADA ZA TANAPA

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma anawajulisha waombaji kazi waliopangiwa kufanya usaili wa mahojiano tarehe **13 Juni,2026** kwa taasisi ya **TANAPA** kuwa, kuna mabadiliko ya eneo la usaili wa mahojiano.

Usaili wa mahojiano utafanyika ofisi za **TANAPA Makao Makuu-Arusha** badala ya Kambi ya JKT Oljoro.

Aidha,tarehe na maelekezo mengine muhimu yatabaki kama yalivyotolewa kwenye tangazo la awali la kuitwa kwenye usaili.

Imetolewa na :
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
26 Mei,2026